



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
TANZANIA INSURANCE  
REGULATORY AUTHORITY**



**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA  
MAMLAKA YA USIMAMIZI  
WA BIMA TANZANIA**

# **INSURANCE TECHNICAL TERMS**

---

## ***ISTILAHU ZA BIMA***

**Version 1.0, July 2025**

***Toleo Na. 1.0, Julai 2025***



**TANZANIA INSURANCE  
REGULATORY AUTHORITY**

**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA  
BIMA TANZANIA**

**INSURANCE TECHNICAL  
TERMS**

**ISTILAH ZA BIMA**

**VERSION 1.0**

**TOLEO Na. 1.0**

**JULY 2025**

**JULAI 2025**

## CONTENTS

|                |    |
|----------------|----|
| Letter A ..... | 1  |
| Letter B ..... | 11 |
| Letter C ..... | 15 |
| Letter D ..... | 26 |
| Letter E ..... | 29 |
| Letter F ..... | 33 |
| Letter G ..... | 38 |
| Letter H ..... | 40 |
| Letter I ..... | 41 |
| Letter J ..... | 49 |
| Letter K ..... | 50 |
| Letter L ..... | 51 |
| Letter M ..... | 55 |
| Letter N ..... | 60 |
| Letter O ..... | 63 |
| Letter P ..... | 64 |
| Letter Q ..... | 74 |
| Letter R ..... | 76 |
| Letter S ..... | 81 |
| Letter T ..... | 86 |
| Letter U ..... | 89 |
| Letter V ..... | 92 |
| Letter W ..... | 93 |
| Letter Y ..... | 94 |
| Letter Z ..... | 95 |

## YALIYOMO

|                |    |
|----------------|----|
| Herufi A ..... | 1  |
| Herufi B ..... | 11 |
| Herufi C ..... | 15 |
| Herufi D ..... | 26 |
| Herufi E ..... | 29 |
| Herufi F ..... | 33 |
| Herufi G ..... | 38 |
| Herufi H ..... | 40 |
| Herufi I ..... | 41 |
| Herufi J ..... | 49 |
| Herufi K ..... | 50 |
| Herufi L ..... | 51 |
| Herufi M ..... | 55 |
| Herufi N ..... | 60 |
| Herufi O ..... | 63 |
| Herufi P ..... | 64 |
| Herufi Q ..... | 74 |
| Herufi R ..... | 76 |
| Herufi S ..... | 81 |
| Herufi T ..... | 86 |
| Herufi U ..... | 89 |
| Herufi V ..... | 92 |
| Herufi W ..... | 93 |
| Herufi Y ..... | 94 |
| Herufi Z ..... | 95 |

| INTRODUCTION                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                 | UTANGULIZI                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                         |
|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| <p>Insurance technical terms have been developed to provide the meaning of various terms used in the insurance industry from insurance perspective. Some words may have different meanings in other contexts, but they are translated here for the specific context of insurance. The process of developing these terms have included Swahili language experts, legal experts, and insurance experts. These terms will be reviewed for three years or when necessary, from time to time.</p> | <p>Istilahi za bima zimeandaliwa ili kutoa maana ya maneno mbalimbali yanayotumika kwenye tasnia ya bima katika mtazamo wa kibima. Baadhi ya maneno huenda yakawa na maana tofauti katika maudhui mengine, lakini yametafsiriwa humu kwa maudhui mahsusi ya kibima. Mchakato wa kutengeneza istilahi hizi umejumuisha wataalamu wa lugha ya Kiswahili, wataalamu wa sheria, pamoja na wataalamu wa bima. Istilahi hizi zitakuwa zikifanyiwa marejeo kila baada ya miaka mitatu au pale itapohitajika ili kuongeza baadhi ya maneno au kuboresha maana kwa maneno yaliyopo au vyote kwa pamoja.</p> |

| ENGLISH                         |                                                                                                                                                                                   | SWAHILI                           |                                                                                                                                                                                                                                   |
|---------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE<br>TECHNICAL<br>TERMS | MEANING                                                                                                                                                                           | ISTILAH ZA<br>BIMA                | UFAFANUZI                                                                                                                                                                                                                         |
| Ab-initio                       | From the beginning or inception of insurance contract                                                                                                                             | -a awali                          | Mwanzoni mwa mkataba wa Bima                                                                                                                                                                                                      |
| Abandonment                     | The act of surrendering ownership of a damaged or lost property to the insurer in exchange for a full claim payment                                                               | Usalimishaji                      | Kitendo cha kuiachia Kampuni ya Bima umiliki wa mali iliyoharibika au iliyopotea kwa kuridhia kupokea malipo kamili                                                                                                               |
| Absolute assignment             | Typically used in insurance contracts, where the policyholder assigns their ownership rights in the policy to another person                                                      | Uhamishaji wa haki za mkatabima   | Hutumiwa katika mikataba ya bima ambapo mkatabima anahamisha haki zake za kibima kwenda kwa mtu mwingine.                                                                                                                         |
| Acceptance of loss form         | Document used by insurance policyholders to accept the amount of the claim payment offered by the insurer. It is used in settling partial losses of the insured's subject matter. | Fomu ya kuridhia malipo ya fidia. | Fomu inayotumiwa na mkatabima kuridhia kiwango cha fidia kutoka kwa kampuni ya bima. Inatumika ikiwa hasara iliyotokea siyo hasara kamili ya kilichokatiwa bima (kilichokatiwa bima kinaweza kurekebishwa na kuendelea kutumika). |
| Accident                        | Unforeseen events that occur suddenly and unintentionally, and which may result in bodily injury, death, loss of property or property damage.                                     | Ajali                             | Matukio yasiyokusudiwa ambayo yanaweza kusababisha majeraha, kifo, upotevu au uharibifu wa mali.                                                                                                                                  |

|                                |                                                                                                                          |                                         |                                                                                                                     |
|--------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Accidental death               | Refers to an unforeseen event that results in loss of life.                                                              | Kifo kwa ajali                          | Kifo kilichosababishwa na ajali.                                                                                    |
| Accidental death benefits      | Benefits paid to the designated beneficiaries after death of a life assured person due to an accident.                   | Mafao ya Kifo kitokanacho na Ajali      | Mafao yanayolipwa kwa wanufaika wateule wa mkatabima aliyeifariki kutokana na ajali.                                |
| Accidental injury benefits     | Benefits that provide financial compensation to an insured person who suffers bodily injuries as a result of an accident | Fidia ya Majeraha yatokanayo na Ajali   | Fidia kwa mkatabima aliyeumia kutokana na ajali.                                                                    |
| Accumulated premium            | Total amount of premiums paid by policyholders for insurance policies in a certain period.                               | Jumla ya ada za Bima zilizokusanywa     | Jumla ya ada za bima zilizokusanywa kwa wakata bima katika kipindi maalumu.                                         |
| Actual cash value              | Fair market value of insured property at the time of loss, less depreciation cost.                                       | Thamani halisi ya mali                  | Thamani halisi ya kilichokatiwa bima wakati wa ajali, ukipunguza gharama ya uchakavu.                               |
| Accredited reinsurance company | Foreign reinsurance companies accredited by authority to transact insurance business with local insurance companies.     | Kampuni za bima mtawanyo zenye ithibati | Kampuni za nje za bima mtawanyo zilizopewa ithibati na mamlaka kufanya biashara ya bima na kampuni za ndani.        |
| Actual risk value              | The actual loss or damage that could result if a particular risk event occurs.                                           | Thamani halisi ya kilichokatiwa bima    | Thamani halisi ya mali ya mkata bima inayoweza kupotea au kupungua likitokea tukio hatari kama ajali, wizi au moto. |
| Actuarial                      | The field of applied mathematical and statistical method to project the occurrence of future events                      | Utathminishaji                          | Uchakataji wa mahesabu na tathmini ya matukio yanayotarajiwa.                                                       |

|                      |                                                                                                                                                                                  |                                |                                                                                                                                                   |
|----------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Actuarial analysis   | The process that uses statistical models and mathematical techniques to assess and manage financial risks.                                                                       | Uchambuzi wa kiutathminishaji  | Mchakato ambao hutumia mifumo ya takwimu na mbinu za hesabu kutathmini na kudhibiti hatari za kifedha                                             |
| Actuarial multiplier | A factor used to adjust the premium or reserve for a particular risk based on its risk characteristics                                                                           | Kizidishi cha kiutathminishaji | Kizidishi kinachotumika kurekebisha ada ya bima au akiba kwa vihatarishi maalum kulingana na sifa za vihatarishi vyake.                           |
| Actuary              | A Professional who applies mathematical and statistical methods to assess and manage risk and uncertainty in various fields, particularly in insurance, finance, and healthcare. | Mtathminishaji                 | Mtaalamu anayetumia mbinu za hesabu na takwimu kutathmini na kudhibiti vihatarishi katika nyanja mbalimbali, hususan katika bima, fedha, na afya. |
| Additional insured   | A person or entity who is granted coverage under an insurance policy, in addition to the named insured who initially purchased the policy.                                       | Mkatabima aliyeongezeka        | Mtu /shirika/taasisi/ kampuni inayongezwa kwenye kinga ya mkataba wa bima ambayo awali haikutajwa kwenye mkataba huo.                             |
| Additional benefit   | Extension or enhancement to the standard coverage provided under a policy.                                                                                                       | Mafao ya ziada                 | Mafao yanayoongezwa katika mkataba wa bima kwa kuongeza malipo ya ada ya bima.                                                                    |
| Additional perils    | Specific causes of loss or events that are not covered under the standard policy but can be added to the policy for an additional premium.                                       | Visababishi hasara vya ziada.  | Ni vihatarishi ambavyo kwa kawaida havikingwi katika mkataba wa bima ila vinaweza kuongezwa katika mkataba wa bima kwa kulipa ada ya ziada.       |

|                                      |                                                                                                                                                          |                                                                   |                                                                                                                                                   |
|--------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Add-on Benefits                      | Also known as riders or endorsements, are optional extensions or enhancements to the standard coverage provided under a policy                           | Mafao ya ziada                                                    | Mafao yanayoongezwa katika mkataba wa bima kwa kuongeza malipo ya ada ya bima.                                                                    |
| Add-on covers                        | Also known as a rider or endorsement, is an optional addition to an insurance policy that provides extra coverage or benefits beyond the standard policy | Kinga ya ziada                                                    | Kinga inayoongezwa katika mkataba wa bima kwa kuongeza malipo ya ada ya bima.                                                                     |
| Adhesion contract                    | Agreement where the terms and conditions are pre-drafted by the insurance company, leaving the customer with no power to negotiate or alter them.        | Mkataba ulioandikwa na upande mmoja                               | Mkataba ambao umetayarishwa na kampuni ya bima, wenye masharti ambayo mteja haruhusiwi kuyabadilisha. Mteja anaweza kukubali au kuukataa mkataba. |
| Admitted assets                      | Assets of an insurance company that are recognized and accepted by state insurance laws in determining the company's financial solvency.                 | Mali Zilizoruhusiwa                                               | Mali za kampuni ya bima zinazotambulika na kukubalika kisheria. Mali hizo hutumika kutathmini uwezo wa ukwasi wa kampuni husika.                  |
| Admitted company                     | Insurance company that has been licensed to operate in a specific line of insurance.                                                                     | Kampuni iliyoruhusiwa kisheria                                    | Kampuni ya bima ambayo imepewa leseni na mamlaka husika kufanya biashara ya bima ndani ya nchi.                                                   |
| Advance loss profit insurance (alop) | Insurance cover designed to protect businesses from financial loss of profit caused by delays in the completion of construction or renovation projects.  | Bima ya hasara iliyosababishwa na kuchelewa kumalizika kwa ujenzi | Kinga ya bima inayofidia hasara (upotevu wa faida) ya kifedha inayotokana na kuchelewa kumalizika kwa miradi ya ujenzi au ukarabati.              |

|                                  |                                                                                                                                                                                                                  |                                        |                                                                                                                                                                            |
|----------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Adverse selection/Anti-selection | Occurs when individuals with a higher risk of making a claim are more likely to purchase insurance than those with a lower risk.                                                                                 | Uchaguzi mbaya wa mkata bima           | Hutokea kwa kampuni ya bima ambapo wakatabima walio katika hatari kubwa zaidi ya kupata hasara hukata bima.                                                                |
| Age related limitation           | Restriction placed on coverage or eligibility based on the applicant's age.                                                                                                                                      | Ukomo wa umri wa mkatabima             | Ukomo wa umri wa mkatabima wa kinga ya bima ya maisha na bima ya afya.                                                                                                     |
| Agency agreement                 | A legally binding contract between an insurance company (the principal) and an individual or organization (the agent) that authorizes the agent to sell and service insurance policies on behalf of the company. | Makubaliano ya Uwakala                 | Ni mkataba wa kisheria kati ya kampuni ya bima na mtu binafsi au shirika (wakala wa bima) ambao unamruhusu wakala kuuza na kusimamia mkataba wa bima kwa niaba ya kampuni. |
| Agent commission                 | Remuneration paid by an insurance company (the principal) to an insurance agent (the agent) for selling and servicing insurance policies on their behalf.                                                        | Kamisheni ya Wakala                    | Malipo yanayotolewa na kampuni ya bima kwa wakala wa bima kwa ajili kutoa huduma za bima kwa niaba yao mikataba ya bima kwa niaba yao.                                     |
| Aggregate deductible             | Deductible that applies to all covered claims incurred during a specific period.                                                                                                                                 | Jumla ya mchango wa mteja kwenye Madai | Mchango wa mteja kwenye madai yote yaliyokingwa, unaotolewa katika kipindi maalumu.                                                                                        |
| Aggregate loss                   | Total amount of claim insurer has incurred for a specific policy or group of policies during a specific period.                                                                                                  | Jumla ya Madai                         | Jumla ya madai ambayo kampuni ya bima imeyapokea na ambayo hayajapokewa katika madai ya mkataba wa bima kwa kipindi maalumu.                                               |

|                                 |                                                                                                                                                                                                                                                                                                     |                                                         |                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                                         |
|---------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Stop-loss reinsurance           | A type of reinsurance where the reinsurer covers the loss of the insurer above a specified limit during a defined period (usually a year). It protects the insurer against unexpectedly high claims                                                                                                 | Kiwango cha Juu cha Madai kinacholipwa na Bima Mtawanyo | Ni aina ya bima mtawanyo ambapo kampuni ya bima mtawanyo hulipa fidia kwa hasara zinazozidi kiwango kilichokubaliwa kwa kipindi fulani (kawaida mwaka mmoja). Inamlinda mtoa bima dhidi ya hasara zisizotarajiwa.                                                                                                                                       |
| Aggregate stop-loss reinsurance | Reinsurance used by insurance companies (cedents) to protect themselves from the financial burden of large, unexpected losses. It involves transferring a portion of the risk associated with exceeding a pre-determined loss threshold (stop-loss limit) to another insurance company (reinsurer). | Kiwango cha Juu cha Madai kinacholipwa na Bima Mtawanyo | Ni aina ya bima mtawanyo inayotumika na kampuni za bima (watawanya bima) kujikinga na mzigo wa kifedha wa hasara kubwa zisizotarajiwa. Bima mtawanyo inajumuisha kuhamisha sehemu ya vihatarishi inayohusiana na kuzidi kiwango cha upotevu kilichopangwa awali (kiwango cha kukomesha hasara) kwa kampuni nyingine ya bima (kampuni ya bima mtawanyo). |
| Agreed Value policy             | A predetermined amount that an insurance company will pay out in the event of a covered loss.                                                                                                                                                                                                       | Thamani ya fidia iliyokubaliwa.                         | Kiasi cha fidia walichokubaliana kampuni ya bima na mkatabima, ambacho kampuni ya bima itawajibika kulipa yatakapotokea matukio yaliokatiwa bima.                                                                                                                                                                                                       |
| Agreed value                    | A value of the subject matter agreed between the parties at the inception of the Insurance Policy                                                                                                                                                                                                   | Thamani iliyokubaliwa                                   | Ni thamani ya kilichokatiwa bima iliyokubaliwa kati ya pande mbili mwanzo mwa mkataba wa bima.                                                                                                                                                                                                                                                          |

|                                      |                                                                                                                                                                                                            |                                         |                                                                                                                                                                                                                              |
|--------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Air freight insurance                | Type of insurance policy specifically designed to protect goods transported by air.                                                                                                                        | Bima ya usafirishaji wa mizigo kwa anga | Mkataba wa bima ya usafirishaji wa mizigo kwa njia ya anga.                                                                                                                                                                  |
| Alteration to the policy             | Any change to the terms and conditions of an insurance policy. This can include changes to the type of coverage, the amount of coverage, the deductibles, the premiums, or any other aspect of the policy. | Marekebisho kwenye mkataba              | Mabadiliko ya vigezo na masharti ya mkataba wa bima. Hii inaweza kujumuisha mabadiliko kwenye aina ya bima, kiasi cha kinga ya bima, Mchango wa mkataba kwenye madai yake, ada za bima au sehemu nyingine yoyote ya mkataba. |
| Alternative dispute resolution (adr) | A method used to resolve disputes between insurance companies and policyholders outside of the traditional court system.                                                                                   | Usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala | Mbinu mbadala zinazotumiwa kutatua migogoro kati ya kampuni za bima na wakatabima nje ya utaratibu wa mahakama                                                                                                               |
| Annuity                              | Contract between an insurance company and an individual that guarantees the individual regular income payments for a specified period or for life                                                          | Malipo ndondondo                        | Mkataba kati ya kampuni ya bima na mkatabima ambao unamuhakikishia mkatabima kupokea malipo ya mara kwa mara kwa muda maalumu au muda wote atakaoishi                                                                        |

|                 |                                                                                                                                                                                                                                                             |                            |                                                                                                                                                                                                                                                                         |
|-----------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Annuitant       | An individual who is entitled to receive regular payments from an annuity contract or a pension plan. These payments are typically made on a monthly, quarterly, or annual basis and can continue for a set period of time or for the annuitant's lifetime. | Mpokeaji malipo ndondondo  | Mkatabima ambaye ana haki ya kupokea malipo ya mara kwa mara kutoka kwa mkataba wa malipo ndondondo au mpango wa pensheni. Malipo haya kwa kawaida hufanywa kila mwezi, robo mwaka, au mwaka na yanaweza kuendelea kwa kipindi maalumu au kwa maisha yote ya mkatabima. |
| Annuity certain | A specific type of annuity that provides guaranteed payments for a predetermined period of time, regardless of the annuitant's life expectancy                                                                                                              | Malipo ndondondo hakika    | Aina maalumu ya malipo ndondondo inayotoa malipo ya uhakika kwa kipindi cha muda uliopangwa awali, bila kujali matarajio ya maisha ya mkatabima.                                                                                                                        |
| Annuity due     | A specific type of annuity where payments are made at the beginning of each period.                                                                                                                                                                         | Malipo ndondondo ya mwanzo | Aina maalumu ya malipo ambayo hufanywa mwanzoni mwa kila kipindi cha mkataba wa malipo ndondondo.                                                                                                                                                                       |
| Arbitration     | A legal process where two or more parties in a dispute agree to have their case heard and decided by a neutral third party, known as an arbitrator, instead of going to court.                                                                              | Uamuzi                     | Mchakato wa kisheria ambapo pande mbili au zaidi zinazohusika katika mgogoro zinakubaliana kusikilizwa na kuamuliwa mgogoro wao na mtu wa tatu asiye fungamana na upande wowote kama njia mbadala ya Kwenda mahakani.                                                   |

|             |                                                                                                                                                                                               |                                     |                                                                                                                                                                                                                         |
|-------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Arbitrator  | A neutral third party who is chosen by two or more parties in a dispute to consider arguments, hear evidence and issue a binding decision that resolves the disagreement.                     | Mwamuzi                             | mtu wa tatu asiye fungamana na upande wowote. ambaye huchaguliwa na pande mbili au zaidi zenye mgogoro kusikiliza ushahidi, kuzingatia hoja, na kutoa uamuzi ambao unatatua mgogoro huo.                                |
| Arson       | Criminal act of malicious or deliberately setting property on fire. Policyholders may commit arson with fraudulent intent of causing property damage so as to receive insurance compensation. | kuchoma moto mali kwa makusudi      | Kitendo cha makusudi cha kuharibu mali kwa moto. Ikithibitika kwamba mkatabima amehusika kwenye uharibifu huo wa mali iliyokatiwa bima ili kujinufaisha na mkataba wa bima, kampuni ya bima haitawajibika kulipa fidia. |
| Assignee    | A person, company, or entity which receives the transfer of property rights and obligations from another party.                                                                               | Mhamishiwa umiliki                  | Mtu, kampuni, au taasisi inayopewa haki na majukumu ya umiliki wa mali kutoka kwa mtu, kampuni au taasisi nyingine.                                                                                                     |
| Assignor    | A person, company, or entity which transfers property rights and obligations to another party.                                                                                                | Mhamisha umiliki                    | Mtu, kampuni, au taasisi inayotoa haki na majukumu ya umiliki wa mali kwa mtu mwingine, kampuni au taasisi nyingine.                                                                                                    |
| Assured     | A person who is entitled to receive benefits out of a life assurance contract.                                                                                                                | Mnufaika wa bima ya maisha          | Mnufaika wa bima ya maisha baada ya kifo cha mkatabima.                                                                                                                                                                 |
| Attestation | Verification of the accuracy and completeness of information provided by the policyholder.                                                                                                    | Uthibitisho wa usahihi na ukamilifu | Kuthibitisha usahihi na ukamilifu wa taarifa zinazotolewa na mkatabima kabla ya kufanya uamuzi ya kumkatia bima.                                                                                                        |

|                       |                                                                                                                                                                     |                                      |                                                                                                                                                                      |
|-----------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Authorized driver     | A person who has been granted permission by the policyholder to drive the insured vehicle.                                                                          | Dereva mwenye ithibati               | Ni mtu ambaye amepewa ruhusa na mkatabima kuendesha gari lililokatiwa bima.                                                                                          |
| Authorized repairer   | A company or individual accredited by the insurance regulator and approved by an insurance company to carry out repairs on insured vehicles                         | Mrekebishaji mwenye ithibati         | Kampuni au mtu binafsi ambaye amepewa ithibati na mamlaka ya usimamizi wa bima kufanya matengenezo ya magari yenye bima.                                             |
| Auto insurance policy | Insurance policy that provides financial protection to individuals or businesses in the event of damage to or loss related to the insured motor vehicle.            | Bima ya vyombo vya moto              | Bima ambayo humkinga mkatabima dhidi ya matukio ya uharibifu au hasara itokanayo na chombo cha moto iliyokatiwa bima.                                                |
| Average clause        | Clause that states the insurance company will only pay a proportion of the loss if the insured value of the property is less than the actual value of the property. | Kifungu cha thamani halisi           | Kifungu cha mkataba kinachoelekeza kwamba kampuni ya bima italipia sehemu tu ya hasara ikiwa thamani ya mali iliyokatiwa bima ni pungufu kuliko thamani yake halisi. |
| Aviation insurance    | A specialized type of insurance designed to cover the risks associated with the operation of aircraft, the people and property involved.                            | Bima ya vyombo vya usafiri wa angani | Bima inayomkinga mkatabima dhidi ya hasara itokanayo na vyombo vya usafiri wa angani ikiwemo uharibifu wa chombo, dhima kwa abiria na mizigo iliyobebwa.             |

| ENGLISH                   |                                                                                                                                                                                                                                                                                     | SWAHILI                  |                                                                                                                                     |
|---------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE TECHNICAL TERMS | MEANING                                                                                                                                                                                                                                                                             | ISTILAH ZA BIMA          | UFAFANUZI                                                                                                                           |
| Bad faith claim           | Occurs when an insurer delays in the processing of a legitimate claim beyond time period consistent with normal insurance industry practice or delay making payment in claim beyond 45 days from the date of receipt of executed discharge voucher without consent of Commissioner. | Madai yaliyo-cheleweshwa | Madai halali ambayo kampuni ya bima imeshindwa kulipa fidia ndani ya muda elekezi wa Mamlaka ya bima.                               |
| Bancassurance             | Mechanism by which banks or financial institutions and insurers collaborate to distribute and market insurance products                                                                                                                                                             | Benkibima                | Mfumo wa benki au Taasisi za kifedha na kampuni za bima hushirikiana katika kusambaza, kutangaza na kuuza bidhaa za huduma za bima. |
| Bancassurance Agent       | Bank or other financial institution licensed by the Authority to conduct bancassurance business.                                                                                                                                                                                    | Wakala wa Benkibima      | Benki au taasisi nyingine ya fedha iliyopewa leseni na Mamlaka kutoa huduma za bima.                                                |
| Bancassurance business    | Provision of insurance products or services by a bank or financial institution on behalf of an insurer                                                                                                                                                                              | Biashara ya Benkibima    | Ufanyaji wa biashara ya bima kupitia benki au taasisi nyingine za fedha kwa niaba ya kampuni ya bima.                               |

|                    |                                                                                                                                                                                   |                                                         |                                                                                                                                                                                                             |
|--------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Barratry           | A deliberate wrongful act committed by the captain or crew of a ship that harms the interests of the ship's owner or cargo owner.                                                 | Uhalifu unaofanywa na wafanyakazi wa chombo cha majini. | Ni kitendo cha uhalifu wa makusudi kinachofanywa na nahodha au mfanyakazi wa vyombo vya majini ambacho kinadhuru maslahi ya mmiliki wa chombo au mizigo.                                                    |
| Beneficiary        | An individual or entity designated to receive the benefits or proceeds from an insurance policy in the event of the insured person's death or other covered event.                | Mnufaika wa bima                                        | Kampuni/taasisi/shirika au mtu aliyeteuliwa kupokea mafao kutoka kwenye mkataba wa bima katika tukio la kifo la mtu aliye kata bima au tukio lingine lililokingwa na bima.                                  |
| Betterment Clause  | A clause that limits the insurer's obligation for repairs or replacements that enhance the condition of the covered property beyond its pre-loss condition.                       | Kifungu cha ukomo wa uboreshaji                         | Kifungu cha mkataba wa bima, ambacho huweka ukomo wa dhima ya kampuni ya bima kurekebisha au kubadilisha mali iliyoharibiwa kwa kiwango ambacho kinaboresha hali yake kuliko ilivyokuwa kabla ya uharibifu. |
| Betterment Charges | A specific type of cost imposed on policyholders when repairs or replacements made after a claim result in the improvement of the insured property beyond its pre-loss condition. | Gharama za uboreshaji                                   | Fedha anazolipa mkata bima baada ya kilichokatiwa bima kutengenezwa na kuwa bora kuliko awali.                                                                                                              |

|                                  |                                                                                                                                                                                                         |                                   |                                                                                                                      |
|----------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Binder                           | A temporary document that evidences the existence of insurance coverage until issuance of the policy.                                                                                                   | Cheti cha muda cha bima           | Waraka wa muda mfupi unaothibitisha uwapo wa Mkataba wa Bima kabla ya kutolewa kwa hati ya mkataba wa bima           |
| Double Insurance          | Situation in which the same property is covered by two or more insurance policies for the same risk.                                                 | Hali ya kitu kukatiwa bima zaidi ya moja. | Hutokea pale ambapo bima zaidi ya moja inakinga kitu kimoja dhidi ya vihatarishi vinavyofanana.                                                    |
| Duty of care              | Legal and ethical responsibility that all parties to a contract have towards one another.                                                            | Wajibu wa uangalifu                       | Jukumu la kisheria na kimaadili ambalo linapaswa kuzingatiwa na kutekelezwa na kampuni ya bima na mkatabima.                                       |

| ENGLISH                      |                                                                                                                                                                         | SWAHILI                                                     |                                                                                                                                                   |
|------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE TECHNICAL TERMS    | MEANING                                                                                                                                                                 | ISTILAH ZA BIMA                                             | UFAFANUZI                                                                                                                                         |
| Effective Date               | Date on which an insurance policy goes into effect or becomes active                                                                                                    | Kuanza kwa mkataba wa bima                                  | Tarehe ambayo mkataba wa bima unaanza kutumika                                                                                                    |
| Employee Dishonesty Coverage | Insurance coverage that protects businesses from financial losses resulting from dishonest or fraudulent acts committed by their employees.                             | Kinga ya mwajiri dhidi ya ukosefu wa uaminifu wa waajiriwa. | Bima inayomlinda mwajiri dhidi ya hasara zinazotokana na vitendo vya udanganyifu, ulaghai au utapeli vinavyoweza kufanywa na wafanyakazi wake.    |
| Employer's liability         | Coverage that protects employers against financial losses arising from claims made by employees or their representatives for work-related injuries, illnesses or death. | Bima ya dhima ya mwajiri                                    | Bima ya kumkinga mwajiri dhidi ya madai ya mwajiriwa au wawakilishi wake; yatokanayo na kuumia, kuumwa au kufariki wakati mwajiriwa akiwa kazini. |
| Endorsement                  | Modification or addition to an insurance policy that alters its terms or coverage                                                                                       | Marekebisho ya mkataba                                      | Marekebisho ya kinga au/na masharti ya mkataba wa bima.                                                                                           |
| Endowment Insurance          | Life insurance policy that provides death benefit if the life assured dies within the contract duration or payment of fixed sum upon policy maturity.                   | Bima ya Majaliwa                                            | Bima ya maisha ambayo hutoa fidia kutokana na kifo cha mkatababima kabla ya mkataba kuisha au kulipa kiasi cha fedha baada ya bima kuiva.         |

|                        |                                                                                                                                                                                                                                                   |                                     |                                                                                                                                                                                                      |
|------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Engineering insurance  | Designed to protect businesses involved in construction, installation, and operation of machinery and equipments, as well as those engaged in other engineering-related activities                                                                | Bima ya uhandisi                    | Bima zinazotoa kinga wakati wa ujenzi, ufungaji na uendeshaji wa mashine na vifaa pamoja na shughuli nyingine zinazohusiana na uhandisi.                                                             |
| Estoppel               | A provision that prevents an insurer or insured from denying a fact or coverage if their previous statements, actions, or conduct led the other party to reasonably believe and rely on it.                                                       | Zuio                                | Kifungu kinachozuia kampuni ya bima au mkatabima kukanusha ukweli, endapo kauli, vitendo au mwenendo wao wa awali ulipelekea upande mwingine kuamini na kutegemea taarifa hiyo.                      |
| Estimated Maximum Loss | Maximum amount of loss that an insurer estimates it could potentially incur from a single event or occurrence                                                                                                                                     | Makadirio ya juu ya kima cha hasara | Kima cha juu cha hasara ambacho kampuni ya bima inakadiria kuweza kutokea kwenye tukio moja.                                                                                                         |
| Ex-gratia payments     | Payments made by an insurance company to a policyholder or claimant out of goodwill rather than a legal obligation.                                                                                                                               | Malipo ya hisani                    | Fidia inayotolewa na kampuni ya bima kwa mkata bima pasipo kuwepo na wajibu wa kisheria                                                                                                              |
| Excess buyback         | Option where the insured is essentially paying an additional premium to the insurance company in return, the insurance company agrees to eliminate the standard excess/deductible amount that the policyholder would normally be responsible for. | Ununuzi wa mchango wa madai         | Kitendo ambacho mkatabima anaongeza kiasi fulani cha malipo kwenye ada ya bima ya msingi kwenda kwa kampuni ya bima kwa lengo la kuondoa kiasi ambacho mkatabima atawajibika kulipa wakati wa madai. |

|                                                    |                                                                                                                                                                                                                  |                                                             |                                                                                                                                                  |
|----------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Excess of loss                                     | Reinsurance arrangement where the reinsurer agrees to cover the insurer upon losses that exceed a certain predetermined amount.                                                                                  | Bima mtawanyo kwa hasara ya ziada                           | Bima mtawanyo inayoilipa kampuni ya bima ziada ya hasara kutokana na kiwango kilichokubaliwa wakati wa kukata bima mtawanyo.                     |
| Excess                                             | Compulsory amount which the policyholder ought to pay in each and every claim, before the insurance company settles the remaining claim amount.                                                                  | Mchango wa mkata bima kwenye madai                          | Kiasi ambacho mkatabima anawajibika kulipa wakati wa madai ya bima kabla ya kampuni ya bima kulipa sehemu yao ya madai hayo                      |
| Exclusion                                          | Explicitly stated situations, conditions, or events, outlining circumstances under which the insurer will not provide coverage or pay a claim upon them.                                                         | Vihatarishi visivyokingwa kwenye mkataba                    | Hali, masharti au vihatarishi vinavyobainishwa kwenye mkataba kwamba kampuni ya bima haitavikinga na madai yatakayosababishwa navyo hayatalipwa. |
| Exaggerated Claim                                  | A claim which has been inflated in a way that the reported extent of loss is quite higher than the loss justified by the actual loss scenario.                                                                   | Madai makubwa kuliko uhalisia                               | Madai ambayo yamekuzwa na mkatabima na kufikia kiasi kikubwa cha hasara kuliko uhalisia wa hasara aliyopata.                                     |
| Exemption of accreditation for regional reinsurers | Situation where certain regional reinsurance companies are granted special permission or relief from a requirement, rule, or obligation from the usual accreditation requirements within the insurance industry. | Msamaha wa ithibati kwa kampuni za bima mtawanyo za kikanda | Hali ambayo kampuni za bima mtawanyo za kikanda hupewa msamaha kwa kutotimiza matwaka ya kisheria ndani ya sekta ya bima.                        |

|                    |                                                                                         |                                      |                                                                         |
|--------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------|
| Express conditions | Specific requirements or conditions that are explicitly stated in the insurance policy. | Masharti yaliyoandikwa               | Masharti yaliyoandikwa kwenye mkataba wa bima.                          |
| Externalization    | Process of transferring risk outside of the country through reinsurance arrangements.   | Upelekaji wa vihatarishi nje ya nchi | Utawanyaji wa vihatarishi nje ya nchi kupitia kampuni za bima mtawanyo. |

| ENGLISH                         |                                                                                                                                                                                                               | SWAHILI                              |                                                                                                                                                                 |
|---------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE<br>TECHNICAL<br>TERMS | MEANING                                                                                                                                                                                                       | ISTILAH<br>ZA BIMA                   | UFAFANUZI                                                                                                                                                       |
| Face Value                      | Stated amount of life insurance coverage                                                                                                                                                                      | Thamani ya mkataba wa bima ya maisha | Thamani halisi ya mkataba wa bima ya maisha ambayo kampuni ya bima ya maisha itawajibika kulipa wakati wa madai                                                 |
| Facultative premium levy        | Charge or fee imposed by the regulatory authority to the amount paid by insurance company to reinsurance company for coverage on a case-by-case basis.                                                        | Tozo ya bima mgawanyo                | Ada iliyowekwa na mamlaka ya udhibiti kwenye ada ya bima mgawanyo                                                                                               |
| Facultative reinsurance         | Reinsurance arrangement where individual risks are considered separately and the insurer has the option to choose whether or not to cede a particular risk whilst a reinsurer has an option to accept or not. | Bima mgawanyo                        | Aina ya bima mtawanyo ambayo kampuni ya bima ina uwezo wa kuchagua baadhi ya vihatarishi vya kutawanya na kampuni ya bima mtawanyo inaweza kukubali au kukataa. |
| Fault system                    | Legal framework used to determine who is at fault in an accident or loss, and consequently, who is responsible for covering the associated damages or losses                                                  | Mfumo wa kubainisha mkosaji          | Mchakato wa kisheria unaotumika kutathmini upande ulio na makosa katika ajali au hasara na anayewajibika kufidia uharibifu au hasara husika.                    |

|                    |                                                                                                                                                                       |                                                            |                                                                                                                                                                |
|--------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Fidelity Insurance | Insurance that provides protection to businesses and employers against financial losses resulting from acts of dishonesty or fraud committed by employees             | Kinga ya mwajiri dhidi ya ukosefu wa uaminifu wa muajiriwa | Aina ya bima ambayo hutoa ulinzi kwa waajiri dhidi ya upotevu wa fedha au mali unaotokana na vitendo vya kukosa uaminifu au ulaghai unaofanywa na wafanyakazi. |
| Financial Loss     | Monetary setback or damage suffered by a person due to a covered event or peril                                                                                       | Hasara za Fedha                                            | Upotevu wa fedha unaotokana na uharibifu wa mali iliyokatiwa bima.                                                                                             |
| Financial Risk     | Potential financial loss that a person may face due to various factors                                                                                                | Kihatarishi cha fedha                                      | Uwezekano wa hasara ya fedha ambayo inaweza kumkabili mtu kwa sababu mbalimbali.                                                                               |
| Fire ignition      | Process or event that leads to the starting or initiation of a fire                                                                                                   | Chanzo cha moto                                            | Tukio linalosababisha kuanza kwa moto                                                                                                                          |
| Fire insurance     | Insurance coverage that provides financial protection to individuals, businesses, and other entities in the event of damage or loss caused by fire and allied perils. | Bima ya Moto                                               | Bima ambayo hutoa ulinzi wa mali katika tukio la uharibifu au hasara inayosababishwa na moto na vihatarishi vingine.                                           |

|                      |                                                                                                                                                              |                                                                                         |                                                                                                                                                                                          |
|----------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Fire separation wall | Structure or barrier designed to prevent the spread of fire from one part of a building to another                                                           | Ukuta wa kuzuia moto usisambae                                                          | Ukuta maalumu wa kuzuia kusambaa kwa moto kutoka sehemu moja ya jengo hadi nyingine                                                                                                      |
| First loss basis     | Insurance arrangements which provide partial coverage for goods and contents. It is applicable where there is low probability of occurrence of a total loss. | Kiwango cha juu utakacho-lipwa kwa hasara                                               | Makubaliano ya bima yanayoruhusu ukataji wa bima kwa thamani ya chini ya kinachokatiwa bima endapo kuna uwezekano mdogo wa hasara kamili kutokea.                                        |
| First loss limit     | Maximum amount the insurer is obliged to pay the policyholder for a covered loss that falls within the specified range.                                      | Ukomo wa fidia/<br>Kiwango cha juu cha fidia ambacho kampuni ya bima itawajibika kulipa | Kima cha juu ambacho kampuni ya bima italipa katika mkataba unaoruhusu ukataji wa bima kwa thamani ya chini ya kinachokatiwa bima, endapo kuna uwezekano mdogo wa kutokea hasara kamili. |
| First loss payee     | A person that is specified in an insurance policy as the first to receive payment for their interest in the event of a covered loss                          | Mfidiwa wa kwanza kwenye madai kabla ya kulipa mwingine                                 | Mtu anayetambuliwa katika mkataba wa bima kuwa wa kwanza kulipwa fidia kutokana na mali iliyokatiwa bima kua na maslahi ya zaidi ya mtu mmoja.                                           |
| Fleet cover          | Single Insurance policy which covers multiple vehicles owned , operated or under a custody of a policyholder                                                 | Bima jumuishi ya magari                                                                 | Kinga ya bima kwa magari mengi yanayomilikiwa na mkataba chini ya mkataba mmoja wa bima.                                                                                                 |

|                   |                                                                                                                                                                                                                                                                      |                                                                                    |                                                                                                                                                                                                                                                             |
|-------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Floating policy   | Insurance policy that provides coverage for property or goods that are frequently changing in terms of value or location                                                                                                                                             | Bima ya mali inayoweza kubadilika.                                                 | Mkataba wa bima ambayo hutoa bima ya mali au bidhaa ambazo hubadilika thamani au eneo la kinachokatiwa bima mara kwa mara.                                                                                                                                  |
| Fortuitous Losses | Losses that occur by chance or accidentally.                                                                                                                                                                                                                         | Hasara zisizokusudiwa                                                              | Hasara itokeayo pasi na kukusudiwa                                                                                                                                                                                                                          |
| Foundering at Sea | When a ship is reported to be lost and not found within a stipulated period of time, it is presumed to be lost due to perils of the sea                                                                                                                              | Dhana ya kupotea kwa Meli                                                          | Meli ikiripotiwa kutoonekana katika kipindi kilichobainishwa na hakuna taarifa zinazoeleza kwamba ipo wapi, basi itakuwa imepotea kutokana na visababishi hasara vya baharini.                                                                              |
| Franchise         | Clause stipulating the threshold amount that the insured will be responsible for any loss not in excess of a stated amount, and the insurance company will be liable for full payment of the loss that equals or exceeds that stated amount up to the required limit | Kiwango cha madai ambacho kikifikiwa kampuni ya bima itawajibika kulipa madai yote | Kifungu kinachoeleza kwamba mkataba ambawajibika kwa hasara yoyote isiyozidi kiasi kilichoainishwa, na kampuni ya bima itawajibika kwa malipo kamili ya hasara ambayo ni sawa au zaidi ya kiasi hicho kilichotajwa hadi kikomo cha malipo kilichobainishwa. |
| Fraud             | Intentional act of deceiving, misrepresenting, or providing false information to an insurance company for financial gain                                                                                                                                             | Udanganyifu                                                                        | Upotoshaji wa makusudi wa taarifa kwa kampuni ya bima ili kujinufaisha isivyo halali.                                                                                                                                                                       |

|                      |                                                                                                                                                                                                                                   |                                                               |                                                                                                                                                                                                              |
|----------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Free-Look Period     | Specified period of time during which a policyholder can review their newly purchased insurance policy, and if dissatisfied, can cancel it without incurring any penalties or charges and have their premium refunded accordingly | Kipindi huru cha mkatabima kufanya mapitio ya mkataba wa bima | Kipindi kilichobainishwa ambacho mkatabima anaweza kukagua mkataba wake mpya wa bima, na ikiwa hajaridhika, anaweza kughairi bila kutozwa malipo au adhabu yoyote na kurejeshewa ada yake ya bima aliyolipa. |
| Freight charges      | Costs associated with the transportation of goods from one location to another                                                                                                                                                    | Gharama za usafirishaji wa mizigo                             | Gharama zinazohusiana na usafirishaji wa bidhaa kutoka eneo moja hadi jingine                                                                                                                                |
| Fronting arrangement | Practice where insurer cedes 100% of risk exposure to another insurer or reinsurer                                                                                                                                                | Upelekaji wa vihasarashi nje ya nchi kwa asilimia zote        | Mpango wa uhamishaji wa vihatarishi kwa asilimia mia moja unaofanywa na kampuni ya bima kwenda kwa kampuni ya bima au bima mtawanyo                                                                          |

| ENGLISH                          |                                                                                                                                                                                                                                             | SWAHILI                                 |                                                                                                                                                                              |
|----------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE<br>TECHNICAL<br>TERMS  | MEANING                                                                                                                                                                                                                                     | ISTILAH ZA<br>BIMA                      | UFAFANUZI                                                                                                                                                                    |
| Gambling                         | Involves games of chance or skill where individuals voluntarily risk money on an uncertain outcome with the hope of winning more money                                                                                                      | Kamari                                  | Michezo ambayo watu huweka fedha kwa hiari kwa lengo la kupata fedha Zaidi.                                                                                                  |
| General average Loss             | Expenditure or Loss incurred consciously while countering a peril for saving the ship or a consignment.                                                                                                                                     | Hasara jumuishi ya uokozi               | Hasara inayotokana na utosaji wa mizigo majini kwa lengo la kuokoa hasara kubwa.                                                                                             |
| General average sacrifice        | Principle of maritime law that essentially establishes that all sea cargo stakeholders evenly share any damage or losses that may occur as a result of voluntary sacrifice of part of the vessel or cargo to save the whole in an emergency | Uchangiaji jumuishi wa Hasara ya uokozi | Kanuni ya usafirishaji kwa njia ya maji ambayo ina wataka wadau wa meli na mizigo kuchangia hasara iliyotokana na utosaji wa mizigo majini kwa lengo la kuokoa hasara kubwa. |
| General Insurance                | Broad category of insurance policies that provide coverage for a wide range of risks and perils, unlike life insurance                                                                                                                      | Bima za Kawaida                         | Aina za mikataba ya bima za kawaida isiyo jumuisha bima za maisha.                                                                                                           |
| Goods in Transit insurance (GIT) | Covers merchandise that is being transported from one location to another by using land transport.                                                                                                                                          | Bima ya usafirishaji wa mizigo          | Kinga ya vihatarishi dhidi ya hasara itokanayo na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya ardhini.                                                                                |

|                         |                                                                                                                                                                             |                                                   |                                                                                                                                        |
|-------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Grace Period            | Extra time given after the premium due date during which the policyholder can still pay the premium without losing coverage or facing a policy lapse                        | Kipindi cha msamaha wa muda wa kulipa ada ya Bima | Muda wa ziada unaotolewa baada ya ukomo wa kulipa ada ya bima , ambapo mteja anaweza kulipa bila kuathiri mkataba wa bima wake.        |
| Gross Premium           | Total amount of premium paid by policyholder to an insurance company for coverage during a specific period before deducting VAT and other expenses                          | Ada ghafi ya Bima                                 | Jumla ya ada ya bima inayolipwa na mkatabima kabla ya kutoa kodi na gharama nyingine.                                                  |
| Group Insurance         | Provides coverage for a group of individuals who are usually affiliated through an employer, organization or association                                                    | Bima za vikundi                                   | Bima ya kikundi cha watu ambacho hutokana na shirika, chama au mwajiri.                                                                |
| Group Personal Accident | Provides coverage for a group of individuals against accidental bodily injuries resulting in death or disablement                                                           | Bima ya kikundi dhidi ya ajali                    | Bima ya kikundi cha watu dhidi ya ajali inayosababisha majeraha, ulemavu au kifo                                                       |
| Guaranteed Insurability | Clause that allows the policyholder to renew insurance policy after specified times or circumstances, without the need for medical examination or evidence of insurability. | Uhakika wa kuhuisha mkataba wa bima               | Kifungu katika mkataba wa bima ambacho kinamuwezesha mkatabima kuhuisha mkataba wake bila ya uthibitisho wa vihatarishi vya afya yake. |

| ENGLISH                      |                                                                                                                | SWAHILI                         |                                                                                                                                      |
|------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE TECHNICAL TERMS    | MEANING                                                                                                        | ISTILAH ZA BIMA                 | UFAFANUZI                                                                                                                            |
| Hazard                       | Things or situations that accelerate the likelihood of loss occurrence or the impact of loss                   | Kichocheo cha vihatarishi       | Vitu au hali inayoweza kuongeza uwezekano wa kutokea kwa hasara au kufanya madhara au hasara kuwa kubwa zaidi                        |
| Heir                         | Individuals who are legally entitled to inherit in the event of death                                          | Mrithi                          | Mtu ambaye ana haki ya kisheria ya kurithi haki ya mkatabima kitokeapo kifo.                                                         |
| Household Insurance          | Type of property insurance that provides coverage for a residential building, contents and legal liability.    | Bima ya jengo la makazi na mali | Aina ya bima ya mali ambayo hutoa kinga kwa nyumba za makazi, vilivyomo ndani ya nyumba na dhima kwa mkatabima dhidi ya mtu wa tatu. |
| Hospitalization              | Situation where an insured individual is admitted to a hospital and receives medical treatment as an inpatient | kulazwa                         | Hali ambayo mkatabima analazwa hospitalini na kupatiwa matibabu.                                                                     |
| Hull and Machinery Insurance | Provides coverage for damage to the ship's hull and machinery.                                                 | Bima ya chombo cha majini       | Bima inayokinga uharibifu wa chombo cha majini.                                                                                      |

| ENGLISH                    |                                                                                                                                                                                                                                                                                                   | SWAHILI                                 |                                                                                                                                                                                                                                         |
|----------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE TECHNICAL TERMS  | MEANING                                                                                                                                                                                                                                                                                           | ISTILAH ZA BIMA                         | MAANA                                                                                                                                                                                                                                   |
| Impairment                 | A physical or mental condition that affects a person's abilities or normal functioning.                                                                                                                                                                                                           | Ulemavu                                 | Hali ya kimwili au kiakili inayoathiri uwezo au utendaji wa kawaida wa mtu.                                                                                                                                                             |
| Implied conditions         | Certain obligations or requirements that are understood to be inherent in an insurance contract, even if they are not explicitly stated                                                                                                                                                           | Masharti yasioandikwa kwenye mkataba    | Masharti ambayo yanaeleweka kuwa ya asili katika mkataba wa bima, hata kama hayajaaainishwa wazi.                                                                                                                                       |
| Inbound Insurance Travel   | A type of insurance policy designed to cover non-residents while they are traveling within a specific country which provides financial protection against unexpected events during the trip, such as medical emergencies, accidents, lost or delayed baggage, and other unforeseen circumstances. | Bima ya raia wa nje<br>Kuingia Nchini   | Aina ya bima ya safari inayotolewa kwa raia wa nje wakati wanaposafiri ndani ya nchi hiyo, ikiwa na Lengo la kutoa ulinzi wa kifedha dhidi ya majanga yasiyotegemewa yanayoweza kutokea wakati wa safari yao.                           |
| Incontestability Provision | A provision in life and disabilities insurance policy, preventing the insurer from voiding the policy or denying a claim based on misstatements or errors in the application after a specified period.                                                                                            | Kifungu cha kutositisha mkataba wa bima | Kifungu katika mkataba wa bima ya maisha na ulemavu kinachozuia kampuni ya bima kubatilisha mkataba au kukataa kulipa fidia kwa misingi ya taarifa zisizo sahihi au makosa yaliyotolewa katika maombi baada ya kipindi kilichoainishwa. |

|                             |                                                                                                                                                                                                                      |                                                                 |                                                                                                                                                                                    |
|-----------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Increase in Cost of Working | A coverage that helps businesses recover additional expenses they may incur to maintain their operations after a covered loss or damage.                                                                             | Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kufuatia uharibifu wa mali | Kinga inayosaidia kurejesha gharama za ziada ambazo zimetumika ili kuendeleza n shughuli baada ya hasara au uharibifu uliokingwa.                                                  |
| Incurred But Not Reported   | Estimated value of claims that have occurred but have not yet been reported to the insurance company                                                                                                                 | Madai yaliyotokea pasi kuripotiwa                               | Makadirio ya madai ambayo yametokea lakini bado hayajaripotiwa kwa kampuni ya bima                                                                                                 |
| Incurred Losses             | Losses that an entity has experienced or accrued during a specific period                                                                                                                                            | Jumla ya hasara iliyopatikana                                   | Hasara ambayo kampuni imepata katika kipindi fulani.                                                                                                                               |
| Indemnification aliunde     | The right of recovery which states that, prior to payment by the insurer, the loss is extinguished by the insured recovering it from the negligent third party whereby the insurer's liability is also extinguished. | Fidia kwa mkatabima kupitia chanzo kingine                      | Kifungu cha mkataba wa bima kinachomruhusu mkatabima kulipwa fidia kutoka kwa mtu wa tatu aliyemsababishia hasara hiyo, hivyo kuondoa wajibu wa kampuni ya bima kulipa fidia hiyo. |
| Indemnity                   | To compensate the insured party for covered losses or damages by restoring the insured to the same financial position they were in before the covered loss occurred, and not to provide a financial gain             | Msingi wa fidia                                                 | Kumrejesha mkatabima katika hali ya fedha aliyokuwa nayo kabla ya hasara iliyokingwa kutokea, na si kumnufaisha.                                                                   |
| Indemnity Period            | The length of time for which benefits are payable under an insurance policy                                                                                                                                          | Kipindi cha fidia                                               | Muda ambao fidia inapaswa kulipwa katika mkataba wa bima.                                                                                                                          |
| Inflated Claim              | Situation where an insurance policyholder exaggerated value about the extent of the loss or damage.                                                                                                                  | Madai makubwa kuliko uhalisia                                   | Hali ambayo mkatabima anataja kiasi kikubwa cha fidia kwenye madai.                                                                                                                |

|                    |                                                                                                                                                                        |                                                              |                                                                                                                                                                |
|                      |                                                                                                                                                                                                                                         |                                                                       |                                                                                                                                                                                                                                                                              |
|----------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Surplus Share Treaty | A type of proportional reinsurance agreement where the ceding insurer retains a predetermined amount of risk (the “retention”) and the reinsurer covers the excess amount, sharing premiums and losses based on the agreed proportions. | Bima mtawanyo ya kwa vihatarishi vinavyozidi uwezo wa kampuni ya bima | Aina ya bima mtawanyo ambapo kampuni ya bima inabakiza viwango vya vihatarishi inavyovihimili na kuhamisha vihatarishi vilivyozidi kwenda kwa kampuni ya bima mtawanyo kwa makubaliano ya kugawana ada ya bima pamoja na hasara zitakazo tokea kwa viwango walivyokubaliana. |
| Surrender Charge     | A fee charged on a life insurance policyholder upon cancellation of life insurance policy.                                                                                                                                              | Tozo ya kusitisha mkataba wa bima ya maisha                           | Tozo inayotozwa na kampuni ya bima kwa mwenye bima ya maisha baada mkatabima kusitisha mkataba wa bima.                                                                                                                                                                      |
| Surrender value      | Amount of money a policyholder receives from the insurance company when they voluntarily cancel (surrender) a life insurance policy before it matures or before death.                                                                  | Thamani ya kusitisha mkataba                                          | Thamani ya pesa inayolipwa na kampuni ya bima kwa mkatabima baada ya kusitisha mkataba kwa hiari kabla ya muda wake au kabla ya kifo.                                                                                                                                        |

| ENGLISH                    |                                                                                                                                                                                                                                            | SWAHILI                                   |                                                                                                                                                           |
|----------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE TECHNICAL TERMS  | MEANING                                                                                                                                                                                                                                    | ISTILAH ZA BIMA                           | UFAFANUZI                                                                                                                                                 |
| Takaful                    | Shariah compliant insurance system of reimbursement or repayment in case of loss, organized in the form of cooperation between a group of participants who pay an agreed contribution to form a fund for mutual assistance and protection. | Takaful                                   | Mfumo wa bima unaozingatia misingi ya sharia ambao unatoa fidia kwa washiriki waliounda ushirika wa pamoja kwa ajili ya kusadiana kwenye majanga na kinga |
| Takaful Operator           | An entity or company that manages Takaful business on behalf of participants .                                                                                                                                                             | Mwendeshaji wa Takaful                    | Tasisi au kampuni inayoendesha biashara ya Takaful kwa niaba ya washiriki.                                                                                |
| Territorial limit          | A specific area or geographical region defined in the terms of insurance contract or policy are valid and enforceable.                                                                                                                     | Ukomo wa eneo la kijografia               | Eneo maalumu au mipaka ya kijiografia inayoainishwa kwenye mkataba wa bima ambapo bima inakuwa hai na halali                                              |
| Third party                | A person who is not a party to the contract.                                                                                                                                                                                               | Mtu ambaye siyo sehemu ya mkataba wa bima | Mtu asiyekuwa sehemu ya mkataba.                                                                                                                          |
| Third Party insurance Only | A policy with cover limited to the insured's liability for death, injury to or damage to the property of third parties.                                                                                                                    | Bima ya vyombo vya moto kwa mtu wa tatu   | Kinga dhidi ya dhima ya mkataba kwa mtu wa tatu alisababishiwa kifo, majeruha au uharibifu mali.                                                          |

|                             |                                                                                                                                                                             |                                                                                        |                                                                                                                                                                                                                   |
|-----------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Third Party, Fire and Theft | A policy with cover limited to the insured's liability for injury to or damage to the property of, third parties and damage of the vehicle by fire or stolen of the vehicle | Bima ya vyombo vya moto inayomfidi mtu wa tatu,mali ya mkatabima dhidi ya moto na wizi | bima iliyodhibitiwa kwa dhima ya mwenye bima kwa kuumiza au kuharibu mali ya watu wengine na uharibifu wa gari kwa moto au kuibiwa kwa gari.                                                                      |
| Third-Party Claims          | Claim paid to persons who are not parties to the contract of insurance                                                                                                      | Madai ya mtu wa tatu                                                                   | Madai kulipwa kwa mtu ambaye si sehemu ya mkataba wa bima                                                                                                                                                         |
| Third-party liabilities     | Liability incurred by the insured to another party either for death,injury or damage of property .                                                                          | Dhima kwa mtu wa tatu                                                                  | Kinga dhidi ya dhima ya mkatabima kwa mtu wa tatu alisabishwa kifo, majeruha au uharibifu mali                                                                                                                    |
| Third Property Damage       | Loss or damage caused to someone else property (the third party) by insured person                                                                                          | Uharibifu wa mali ya Mtu wa tatu                                                       | Hasara au uharibu wa mali ya mtu wa tatu uliosababishwa na mkata bima.                                                                                                                                            |
| Tied selling                | A practice where an insurance provider or seller conditions the sale of one insurance product on the purchase of another product or service offered by the same provider.   | Mauzo fungamano                                                                        | Inamaanisha kitendo ambacho muuzaji au kampuni ya bima anaweka sharti la kuuza bidhaa moja ya bima kwa kununua bidhaa nyingine au huduma inayotolewa na mtoa huduma huyu.                                         |
| Total Loss                  | A loss of subject matter of insurance such that is totally lost, destroyed or damaged beyond economic repair / A loss that gives rise to payment of the full sum insured.   | Hasara yote ya kilichokatiwa bima                                                      | Uharibifu wa kilichokatiwa bima kama vile kupotea kabisa, kuharibiwa au kuharibiwa zaidi ya ukarabati wa kiuchumi / Hasara ambayo inapelekea mkatabima kulipwa kiwango walichoandikishiana wakati wa kukata bima. |

|                         |                                                                                                                                                                                 |                            |                                                                                                                                                                                          |
|-------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Towing charges          | Expenses for securing disabled vehicle from a public or private road area by attaching, lifting, pulling or dragging and storing such vehicles in a secure facility or location | Gharama za kuvuta gari     | Gharama za kuondoa gari lililoharibika kutoka eneo la barabara ya umma au ya kibinafsi kwa kushikilia, kuinua, kuvuta na kuhifadhi kwenye kituo au eneo salama.                          |
| Towing disabled vehicle | Removing a disabled vehicle from a public or private road area by attaching, lifting, pulling or dragging and storing such vehicles in a secure facility or location            | Kuvuta gari lililoharibika | Kitendo cha kuondoa gari lililoharibika kutoka eneo la barabara ya umma au ya kibinafsi kwa kushikilia, kuinua, kuvuta na kuhifadhi kwenye kituo au eneo salama.                         |
| Transfer of Ownership   | Ownership of a thing is passed from one person to another                                                                                                                       | Uhamishaji wa umiliki      | Kuhamisha haki za umiliki wa kitu kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine                                                                                                                     |
| Travel Insurance        | A type of insurance that protects policy holders from financial losses due to unexpected events during a trip.                                                                  | Bima ya msafiri            | Aina ya bima inayotolewa kwa madhumuni ya kuwalinda wasafiri dhidi ya hasara au usumbufu unaoweza kusababishwa na matukio yasiyotabirika wakati wa safari, ndani ya nchi au nje ya nchi. |
| Treaty Reinsurance      | Reinsurance under contracts (treaties) relating to specific class of insurance                                                                                                  | Mkataba wa Bima mtawanyo   | Mkataba wa bima mtawanyo ambao wanakuwa na makubaliano ya awali ya kuinga aina ya bima                                                                                                   |
| Trust Account           | A legal arrangement in which the grantor allows a third party, the trustee, to manage assets on behalf of the beneficiaries of the trust.                                       | Akaunti ya Dhamana         | Mpango wa kisheria ambapo mtoaji huruhusu mhusika mwingine, mdhamini, kusimamia mali kwa niaba ya wanufaika wa amana.                                                                    |
| Turnaround Time (TAT)   | Time from the submission of a process for execution to the return of the output of that process.                                                                                | Muda wa kushughulika madai | Mwongozo wa muda tangu uwasilishaji, Mchakato wa utekelezaji hadi mwisho wa madai.                                                                                                       |

| ENGLISH                     |                                                                                                                                                                                               | SWAHILI                               |                                                                                                                                                                                            |
|-----------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE TECHNICAL TERMS   | MEANING                                                                                                                                                                                       | ISTILAH ZA BIMA                       | UFAFANUZI                                                                                                                                                                                  |
| Umbrella Policy             | A type of extra liability coverage that provides additional protection beyond the limits of policyholders' existing insurance policies, such as motor, homeowners or renters insurance        | Bima Jumuishi                         | Aina ya bima inayoongeza kinga ya ziada kwa mkatabima pale ambapo fidia ya bima iliyopo (kama ya gari au nyumba) haitoshi kufidia madhara makubwa yanayotokana na madai ya kisheria.       |
| Underinsurance              | Situation where the insured subject matter is insured for the value which is less than its actual value                                                                                       | Kinga ya bima chini ya thamani halisi | Hali ya <b>kukata bima kwa kiwango cha chini</b> kuliko thamani halisi ya mali inayokatiwa bima                                                                                            |
| Underwriter                 | A professional or entity responsibility for evaluating risks and determining the terms, conditions and pricing of an insurance policy                                                         | Mwandikishaji wa bima                 | Ni mtu ambaye anachakata maombi ya bima kwa kuzingatia taarifa za mteja ikiwa ili kuamua bima itatolewe kwa mashariti gani na kiwango gani cha ada ya bima                                 |
| Underwriting                | The process of assessing, evaluating, selecting and determining either to accept or reject an applicant for insurance.                                                                        | Uandikishaji wa bima                  | Ni mchakato wa kutathmini, kuchambua, na kuamua kama maombi ya bima yanapaswa kukubaliwa au lukataliwa .                                                                                   |
| Underwriting considerations | Specific requirements and standards used by insurance companies or underwriters to evaluate the insurability of applicants and assess the risks associated with providing insurance coverage. | Vigezo vya kuandikisha Bima           | Mahitaji na viwango mahususi vinavyotumiwa na makampuni ya bima au waandishi wa chini kutathmini kutoweza kulipwa kwa waombaji na kutathmini hatari zinazohusiana na kutoa huduma ya bima. |

|                          |                                                                                                                                                                                                                                                                                         |                                              |                                                                                                                                                                                                                                                                                      |
|--------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Underwriting profit      | Refers to the profit earned by an insurance company from its underwriting activities. It is the difference between the premiums collected from policyholders and the expenses incurred in providing insurance coverage, including claim payments, administrative costs, and commissions | Faida ipatikanayo na uandikishaji wa Bima    | Faida inayopatikana na kampuni ya bima kutokana na shughuli zake za uandikishaji wa bima. Ni tofauti kati ya malipo yanayokusanywa kutoka kwa wakatabima na gharama zinazotumika katika kutoa huduma ya bima, ikiwa ni pamoja na malipo ya madai, gharama za usimamizi na kamisheni. |
| Unearned premium         | A premium in respect of insurance where risk has never attached. Where the risk has attached that part of the premium that relates to the period of insurance still to run.                                                                                                             | Ada ya bima iliyosalia                       | ada ya bima ambapo hatari muda wake haujapita. Inahusiana na kipindi cha bima ambacho bado kinaendelea.                                                                                                                                                                              |
| Unearned premium reserve | A fund kept by insurer to provide for the claim that may arise in the future under insurance policies that are still in course                                                                                                                                                          | Amana ya ada ya bima iliyosalia              | Fedha zinazotengwa na kampuni ya bima ili kulipa madai ambayo yanaweza kutokea katika siku zijazo chini ya mikataba ya bima ambayo ipo hai                                                                                                                                           |
| Unforeseen               | Events, circumstances, or conditions that are unexpected, unintended, and not anticipated by the insured party                                                                                                                                                                          | Isiyotarajiwa                                | Hali au Matukio ambayo hayakutarajiwa na wala hayakupangwa kutokea na mkatabima                                                                                                                                                                                                      |
| Uninsurable Risk         | A risk that no insurer will accept . This may be because the hazard is too great or can not be quantified.                                                                                                                                                                              | Kihatarishi kisicho na sifa ya kukatiwa bima | Kihatarishi ambacho hakuna kampuni ya bima itakubali kukikinga. Hii labda kwa sababu hatari ni kubwa sana au haiwekani kuhesabiwa.                                                                                                                                                   |
| Uninsured Loss           | Are those losses that an insured may suffer that are not directly covered by a policy of insurance relevant to an insured event.                                                                                                                                                        | Hasara isiyokingwa bima                      | Mkatabima anaweza kupata hasara ambazo hazihusiani moja kwa moja na kilichokingwa na mkataba wa bima.                                                                                                                                                                                |

|                                     |                                                                                                                                                                                        |                                 |                                                                                                                                    |
|-------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Uninsured Perils                    | A cause of loss or damage that is not covered by an insurance policy                                                                                                                   | Vihatarishi visivyo kingwa bima | Kisababishi cha hasara ambacho hakijakingwa na mkataba wa bima                                                                     |
| Universal health insurance (UHI)    | All people have access to the full range of quality health services they need, when and where they need them, without financial hardship.                                              | Bima ya afya kwa wote           | Watu wote wanapata huduma kamili za afya bora wanazohitaji, wakati na mahali wanapozihitaji, bila matatizo ya kifedha.             |
| Utmost Good Faith (Uberrimae Fidei) | The common law duty upon both parties in an insurance contract to reveal all material information to the other party, whether or not such information has been specifically requested. | Uaminifu uliotukuka             | Pande zote mbili katika mkataba wa bima kuweka wazi taarifa zote muhimu kwa upande mwingine, iwe taarifa kama hiyo imeombwa au la. |

| ENGLISH                         |                                                                                                                                                                                                                                                                                   | SWAHILI                             |                                                                                                                                                                                                                                      |
|---------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE<br>TECHNICAL<br>TERMS | MEANING                                                                                                                                                                                                                                                                           | ISTILAH ZA<br>BIMA                  | UFAFANUZI                                                                                                                                                                                                                            |
| Valued Policy                   | An insurance agreement where the insurer and insured agree on the value of the insured item at the time the policy inception, and this agreed-upon value is what the insurer will pay in the event of a covered loss, regardless of the actual loss suffered by the policyholder. | Bima inayoainisha kiwango cha fidia | Aina ya mkataba wa bima ambapo kampuni ya bima na mkatabima wanaafikiana kiwango cha fidia wakati wa kukata bima. Iwapo hasara itatokea, kampuni ya bima italipa thamani hiyo bila kuzingatia thamani halisi ya hasara itakayotokea. |
| Void policy                     | Insurance policy that is considered invalid from the beginning due to misrepresentation or non-disclosure by the policyholder                                                                                                                                                     | Mkataba Batili                      | Mkataba wa bima ambao hautambuliki kisheria tangu mwanzo wa mkataba kwa sababu ya mkatabima kutoweka wazi taarifa muhimu za vihatarishi.                                                                                             |
| Voluntary deductible            | Deductible in which insured agrees to bear in consideration of a reduction of a premium                                                                                                                                                                                           | Kikomo cha hiari cha Mkatabima      | Kiwango ambacho mkatabima anakubali kugharamia kabla kampuni ya bima haijatoa fidia, kwa lengo la kupunguza gharama ya malipo ya bima                                                                                                |
| Voyage Policy                   | Provides coverage for losses due to unforeseen risks to cargo during a specific voyage.                                                                                                                                                                                           | Bima ya safari ya majini            | Mkataba wa bima unaotoa kinga kwa mizigo dhidi ya hasara zitokanazo na vihatarishi visivyotarajiwa wakati wa safari za majini.                                                                                                       |

| ENGLISH                       |                                                                                                                                                       | SWAHILI                                                        |                                                                                                                                          |
|-------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE TECHNICAL TERMS     | MEANING                                                                                                                                               | ISTILAH ZA BIMA                                                | UFAFANUZI                                                                                                                                |
| Waiting period                | Specific time that must pass after a policy begins before the insured can claim or receive certain benefits                                           | Kipindi cha kusubiria                                          | Muda maalum ambao mkatabima husubiri kudai au kupokea mafao yake.                                                                        |
| Waiver                        | Voluntary giving up of a known right or a condition in the insurance contract, either by the insurer or the insured.                                  | Msamaha                                                        | Kitendo cha mkatabima au kampuni ya bima kusitisha haki au masharti yaliyofafanuliwa ndani ya mkataba wa bima baada ya kuyatambua rasmi. |
| Warranty                      | A binding promise or condition stated in the insurance policy made by the insured that certain facts are true or that certain conditions will be met. | Ahadi ya mkatabima                                             | Sharti katika mkataba wa bima ambapo mkata bima anakubali kuwa taarifa fulani ni za kweli au kwamba atatimiza masharti maalum.           |
| Weather index-based insurance | Insurance against a loss caused by adverse weather conditions                                                                                         | Bima ya mazao dhidi ya vihatarishi vitokanavyo na hali ya hewa | Bima dhidi ya hasara inayosababishwa na hali mbaya ya hewa                                                                               |
| Whole Life Insurance          | A type of life insurance that covers the assured for their entire life and guarantees a death benefit to beneficiaries.                               | Bima ya muda wote wa Maisha ya mkata bima                      | Aina ya bima ya maisha inayomlinda mkatabima kwa kipindi chote cha maisha yake, na kutoa fidia ya kifo kwa wategemezi.                   |
| Work-related risk             | Hazards in the workplace occur when the working environment can cause injury, illness or death.                                                       | Vihatarishi mahali pakazi                                      | Visababishi vya Vihatarishi katika mazingira ya kazi vinavyoweza kusababisha majeraha, magonjwa au kifo.                                 |

| ENGLISH                         |                                                                                                                                                                                                                                                                      | SWAHILI                |                                                                                                                                                                                                                                                     |
|---------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE TECHNICAL TERMS       | MEANING                                                                                                                                                                                                                                                              | ISTILAH ZA BIMA        | UFAFANUZI                                                                                                                                                                                                                                           |
| Yacht Insurance                 | A specialized type of marine insurance that provides coverage for boats and yachts used for recreational purposes, racing or other private activities against financial losses resulting from damage to the vessel, theft, liability claims and other related risks. | Bima ya Jahazi         | Aina ya bima ya majini mahsusi kwa ajili ya jahazi zinazotumika kwa burudani, mashindano au shughuli binafsi, inayotoa kinga dhidi ya hasara ya kifedha inayotokana na uharibifu wa chombo, wizi, madai ya dhima, na hatari nyingine zinazohusiana. |
| Yearly renewable term insurance | A type of life assurance that provides coverage for one year at a time and can be renewed annually without a medical exam, though the premium increases each year as the assured gets older.                                                                         | Bima ya muda mfupi     | Bima ya maisha ya muda mfupi ambapo inamruhusu mkatabima kuuhisha/ rejesha bima yake baada ya kuisha kipindi walichokubaliana awali ada yake huongezeka kwa kufuata umri.                                                                           |
| York - Antwerp rules            | A set of internationally accepted guidelines used in marine insurance to govern the principles of General Average — the sharing of losses when cargo, ship, or expenses are deliberately sacrificed or incurred to save a maritime venture in danger.                | Kanuni za York-Antwerp | Mwongozo unaokubalika kimataifa unaotumika katika bima ya majini kudhibiti utosaji mizigo.                                                                                                                                                          |

| ENGLISH                         |                                                                                                                | SWAHILI            |                                                                                               |
|---------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------|
| INSURANCE<br>TECHNICAL<br>TERMS | MEANING                                                                                                        | ISTILAH<br>ZA BIMA | UFAFANUZI                                                                                     |
| Zoning                          | Process of classifying geographical areas based on risk exposure for underwriting and premium rating purposes. | Ukanda             | Kugawanya maeneo katika kanda kwa lengo la kutozai bei ya bima kwa kadri vihatarishi vilivyo. |

|          |                                                                                                                                                                                                                                                                                                |        |                                                                                                                                                                                                                                                                  |
|----------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Approval | <div>Approved by:</div> <div></div> <div>.....</div> <div>Dr. Baghayo A. Saqware</div> <div><b><u>COMMISSIONER OF</u></b><br/><b><u>INSURANCE</u></b></div> <div><b>Date:</b> 30<sup>th</sup> July 2025</div> | Idhini | <div>Imeidhinishwa na:</div> <div></div> <div>.....</div> <div>Dkt. Baghayo A. Saqware</div> <div><b><u>KAMISHNA WA BIMA</u></b></div> <div><b>Tarehe:</b> 30 Julai 2025</div> |
|----------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|

**KIAMBATANISHO / APPENDIX**

**FOMU YA KUTOA MAONI KUHUSU ISTILAHU ZA BIMA  
(“INSURANCE TERMINOLOGY FEEDBACK FORM”)**

Maelezo / Introduction:

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inakaribisha maoni ya wadau kuhusu istilahi za bima zilizotolewa katika chapisho hili. Maoni haya yatasaidia kuboresha ufasaha, uelewa na matumizi ya istilahi hizi katika sekta ya bima nchini.

*(The Tanzania Insurance Regulatory Authority (TIRA) welcomes feedback from stakeholders on the insurance terms presented in this publication. Your input will help improve clarity, understanding, and applicability of these terms within the insurance sector.)*

Tafadhali jaza fomu hii na uitume kwa barua pepe:  
(“ Please complete this form and send it via email to:”)  
coi@tira.go.tz, cc mweni.almas@tira.go.tz

**1. MAELEZO YA PENDEKEZO / DETAILS OF YOUR SUGGESTION**

Kipengele (*Field*) Jibu / Response

Neno linalohusika (*Term concerned*)

Maana iliyopo (*Existing definition*)

Maoni au tafsiri mpya (*Your suggestion*)

Sababu ya pendekezo hilo  
(*Justification for your suggestion*)

**2. MAONI YA ZIADA / ADDITIONAL COMMENTS (Kama yapo / If any):**

.....

.....

.....



**TIRA BIMA HOUSE**  
**Mtaa wa TIRA, Njedengwa**  
**S.L.P 2987 DODOMA**  
**Tovuti: [www.tira.go.tz](http://www.tira.go.tz)**  
**Baruapepe: [coi@tira.go.tz](mailto:coi@tira.go.tz)**